# STANDARD FIVE MID-TERM 3 EXAMS

# 2016

## KISWAHILI

Coordinated by KENPRO,
Macjo Arcade, 4th Floor, Suite 15E,
Off Magadi Road, Ongata Rongai |Tel: +254202319748 |
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website:www.schoolsnetkenya.com

# KISWAHILI

MUDA: SAA1 DAKIKA40

**Soma kifungu kifuatacho, kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa maneno manne hapo chini chagua neno lifaalo kati ya yale uliyopewa.**

Nilikuwa na umri wa ___1___ ishirini na ___2___ maisha ___3___ bado ___4___ na matumaini yake yalikuwa ___5___ sana. Katika afya nilikuwa nimejaa utomvu wa uzima katika moyo furaha. Kichwa ___6___ bado kuota ___7___ na ugonjwa ___8___ mbali na mwili. Uchovu ulikuwa kitu ___9___ kukiona mwilini. Nilikuwa katika mwanzo tu ___10___ maisha. Bado sijafika katikati ___11___ mwisho wake. Kurasa ___12___, maisha yangu yaliyopita yalikuwa ___13___ na matendo haba yaliyoandikwa juu yake katika wakati ___14___ yalikuwa hayawezi kuwatamanisha wengine huyanakili wala hunidhisha mimi ___15___.

| | A | B | C | D. |
|---|---|---|---|---|
| 1. | mwaka | miaka | miyaka | myaka |
| 2. | misaba | misita | mitisa | saba |
| 3. | yalikuwa | ilikuwa | zilikuwa | ulikuwa |
| 4. | mpya | vipya | mipya | mapya |
| 5. | mengi | mingi | nyingi | vingi |
| 6. | kilikuwa | kulikua | ilikuwa | ulikuwa |
| 7. | umbu | mbu | mvi | nvi |
| 8. | yalikuwa | ilikuwa | kilikuwa | ulikuwa |
| 9. | ngeni | geni | kigeni | mgeni |
| 10. | wa | ya | la | cha |
| 11. | wala | ila | ili | bila |
| 12. | ya | za | wa | la |
| 13. | mingi | vichache | mengi | chache |
| 14. | ya | wa | za | cha |
| 15. | mwenye | wenyewe | yenyewe | mwenyewe |



Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

**Chagua jibu sahihi zaidi katika maswali 16 - 30.**

16. Wingi wa kiti hiki ni changu ni ____
A. viti hivi ni vyangu.
B. viti hivi ni vyetu.
C. viti hivi ni zetu.
D. viti hivi ni vyenu.

17. Kitendawili : Nyama nje ngozi ndani.
A. moyo B. embe
C. firigisi D. samaki

18. Kanusha : Miti imeanguka
A. miti haikuanguka.
B. miti hayajaanguka.
C. miti haijanguka.
D. miti haianguki.

19. Alamsiki ? Jibu lake ni ________
A. alamsiki B. buriani
C. binuru D. karibu

20. Badala ya kusema mtoto anayekuja pia tunaweza kusema
A. Mtoto akujaye.
B. Mtoto anayekujaye.
C. Mtoto ajaye.
D. Mtoto ajae.

21. Jina langu jingine ni bombo. Mimi ni vazi gani?
A. Suruali B. Kaptura
C. Kaputula D. Surupwenye

22. Mtoto mdogo ameanguka vibaya. Katika sentensi hii, Kivumishi ni
A. mtoto B. ameanguka
C. mdogo D. vibaya

23. Chagua sentensi iliyo sanifu zaidi.
A. Wageni wakulao wali ni hawa.
B. Wagonjwa wakufao hospitalini ni wengi.
C. Ng'ombe wanywao maji wamelala.
D. Wanafunzi wakujao shuleni ni wale.

24. Baada ya mayai kutagwa
A. huaguliwa B. huunguliwa
C. huangaliwa D. huanguliwa

25. Chagua jibu lenye viulizi sahihi
Milango _______ na funguo ______ hupatikana hapo?
A. ipi, zipi B. zipi, ipi
C. zipi, zipi D. yapi, ipi

26. Majuto ni mjukuu huja kinyume ni ______
A. tashbihi B. takriri
C. methali D. kitendawili

27. Chagua sentensi yenye matumizi sahihi ya - amba.
A. Mwalimu ambaye anayetufurahisha ni huyu.
B. Mwalimu ambao anatufundisha ni huyu.
C. Mwalimu ambaye atatufundishaye ni huyu.
D. Mwalimu ambaye anatufundisha ni huyu.

28. Kifu kizima kina sudusi ngapi?
A. Tatu B. Sita
C. Saba D. Tano

29. Chagua sentensi iliyo na matumizi sahihi ya - enye na enyewe.
A. Mtu mwenye alikuja alienda mwenyewe.
B. Watu wenye wanakula sana ni wenyewe hushiba.
C. Mtoto mwenye ana kitabu alikisoma mwenyewe.
D. Mtoto mwenye kitabu alikisoma mwenyewe.

30. Mwalimu _______ wanafunzi maswali rahisi.
A. aliwapea B. alipeana
C. alipatiana D. aliwapa



Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

Soma kisa kifuatacho kisha ujibu maswali 31 - 40.

Ulevi una vituko vyake . Sugu na Sungu walikuwa na mazoea ya kunywa pombe pamoja . Sugu alikuwa mlevi kuliko Sungu. Lakini ulevi ni ulevi tu hata ukinywa kidogo, wewe bado ni mlevi tu.

Siku moja Sungu alikunywa pombe akamaliza. Akasema, "Rafiki yangu Sugu, mimi ninaenda nyumbani. Watoto wangu wapo nyumbani. Wamefunga shule. Naenda nikakae nao ili tuongee!" Aliondoka saa mbili usiku. Alipokuwa akienda, alipitia kwenye kichocho cha katikati ya mahali penye makaburi. Bahati mbaya, Sungu aliteleza akatumbukia ndani ya kaburi lililokuwa wazi. Lilichimbwa ili kuzika maiti kesho yake. Alipojaribu kutoka, alishindwa. Ujanja ukaisha na ulevi ukaloweka.

Usiku saa tano, Sugu naye alianza mwendo kuelekea nyumbani. Alilewa na kupitia kichocho cha makaburi akiimba nyimbo za ulevi. Kufika pale penye kaburi wazi, alitumbukia ndani kwa vishindo, " kubi" Alishtuka sana alipomwangukia mtu - maiti labda. Pombe ikamloka akilini. Alijaribu kutoka ili asikae na maiti yule, lakini alishindwa. Akasikia sauti ikisema, "Usijisumbue ndugu yangu, hata mimi nimeshindwa kutoka. Mimi na wewe leo zote tu maiti!

31. Sugu na Sungu walizoea ______
    A. kulewa sana.
    B. kuuza pombe.
    C. kunywa pombe gengeni.
    D. kutembea pamoja.

32. Siku moja Sungu
    A. alilewa sana akaanguka
    B. alibaki gengeni.
    C. alirudi nyumbani mapema.
    D. alimwacha Sugu gengeni.

33. Ni watoto gani waliofunga shule?
    A. Watoto wa Sungu. B. Watoto wa Sugu.
    C. Watoto wa gengeni. D. Watoto walevi.

34. Sungu aliondoka gengeni saa mbili ili aende wapi?
    A. Makubirini.
    B. Kichochoroni.
    C. Kwa maiti.
    D. kuongea na watoto wake.

35. Sungu alipoteleza na kutumbukia kaburini
    A. alishindwa kutoka.
    B. alipata maiti.
    C. alimngojea Sugu.
    D. alilewa sana.

36. Kaburi lililokuwa wazi lilikuwa lakumzika
    A. Sugu B. Sungu
    C. maiti D. mlevi

37. Kwa nini Sugu alishtuka alipotumbukia kaburini
    A. alimkuta maiti
    B. alimwona Sungu
    C. alijua ameangukia maiti
    D. alilewa sana

38. Sauti ambayo Sugu alisikia kaburini ilikuwa ya
    A. Sungu B. Maiti
    C. Shetani D. Mlevi

39. Mwishowe kwa maoni yako unadhani vipi
    A. walevi na maiti wote ni sawa.
    B. maiti na walevi wote wanapendana.
    C. Sugu na Sungu wote walila kaburini usiku kucha.
    D. walevi wote wawili walitoka kaburini usiku huo huo.

40. Kichwa kifaacho habari hii ni ______
    A. vituko vya ulevi.
    B. kaburi la walevi.
    C. walevi na maiti.
    D. ulevi ni hatari.



Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

**Soma habari hii kisha ujibu maswali 41 - 50.**

Vijiji vya gatuzi vimebaki kama visiwa na wakazi wote hawawezi kuondoka kwenda mahali popote kwa sababu ya kuzingirwa na mafuriko.

Tangu mvua kubwa ianze kunyesha sehemu zote, wananchi hawajapokea misaada yoyote ya usafiri, vyakula wala dawa za kujikinga na kujitibu kutokana na magonjwa kama vile kichocho malaria homa ya matumbo na kuhara. Kwa muda mrefu sana mvua kubwa imekuwa ikinyesha katika magatuzi yote ya nchi yetu.

Kulingana na maelezo ya wataalam wa hali ya mazingira, mafuriko hayo yamesababishwa na hatari za kuharibu mazingira kote nchini. Watu wanakata miti ovyoovyo na kulima kila sehemu. Hawajui kwamba mizizi ya miti hiyo ndiyo inayoshikilia udongo na kuzuia mmomonyoko. Pia watu wengine wanalima hadi kando kando ya mito na kusababisha kuwapo kwa udongo laini karibu na kingo za mto.

Tatizo jingine ni kujenga kila mahali bila kuyajali mazingira. Wakati umefika ambapo lazima tuyatunze mazingira vizuri la sivyo, majanga yatakuwa mengi. Ni janga ni jangamizi , huangamiza.

**41.** Vijiji vimebaki kama visiwa kwa sababu
A. ya kuzungukwa na mafuriko.
B. wakazi hawawezi kutoka.
C. hawajapokea misaada.
D. hakuna dawa.

**42.** Tangu mvua ianze kunyesha
A. wakazi wamekata miti.
B. magonjwa yamezidi.
C. hakuna magonjwa.
D. wataalam wamekuja.

**43.** Mvua kubwa imekuwa ikinyesha kwenye
A. baadhi za wilaya
B. vijiji vingine.
C. kila gatuzi.
D. sehemu fulani za nchi.

**44.** Wataalam wa mazingira wanasema
A. mafuriko ni hatari.
B. watu wanakata miti.
C. mvua itazidi.
D. uharibifu mazingira ni hatari.

**45.** Mizizi ya miti ______
A. husaidia kushikilia udongo.
B. husababishwa mafuriko.
C. husababisha udongo kuwa laini.
D. ni dawa ya tumbo.

**46.** Tunaambiwa kwamba watu wengine wanalima
A. kwenye mito.
B. ili kuzuia udongo.
C. kuzuia janga la mafuriko.
D. kujifurahisha.

**47.** Mara nyingi mafuriko hutokea nyakati za
A. masika B. kiangazi
C. vuli D. kipupwe

**48.** Katika taarifa hii neno wakazi lina maana
A. wafanyi kazi
B. wanakazi
C. wenyeji
D. wakazi

**49.** Tuyatunze mazingira ili
A. tujenge mbali na mito.
B. ili tuzuie udongo.
C. kuzuia janga la mafuriko.
D. tusilime.

**50.** Taarifa hii ni kuhusu janga la ______
A. mazingira
B. mafuriko
C. miti
D. magonjwa



Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27